

UAINISHAJI WA MOFIMU KATIKA SENTENSI ZA KISWAHILI-KIINGEREZA

Shadrack Kirimi Nyagah, Iribi Mwangi & Basilio Gichobi Mungania

Ikisiri

Makala hii inalenga kuainisha mofimu katika sentensi zinazotokana na uhamishaji msimbo unaohusu lugha za Kiswahili na Kiingereza. Utafiti huu unaongozwa na Modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi ya Myers-Scotton (1993) na modeli ya M-4 ya Myers-Scotton & Jake (2000). Kando na kuainisha mofimu katika sentensi za Kiswahili-Kiingereza, kazi hii pia inachunguza majukumu yanayotekelizwa na lugha za Kiswahili na Kiingereza katika sentensi moja. Data ya utafiti huu imetokana na mazungumzo ya kawaida kutoka katika vipindi viwili vinavyoigizwa kwenye runinga ya NTV- Kenya ambavyo ni “The Wicked Edition” na “The Real Househelps of Kawangware.” Matokeo ya uchunguzi huu yanadhihirisha kwamba mofimu katika sentensi za Kiswahili-Kiingereza zinaweza kuainishwa katika matapo manne makuu, yaani: mofimu za kidhana, mofimu za kimfumo za mapema, mofimu mfumo za kidaraja na mofimu mfumo za nje. Kila aina ya mofimu hutekeleza jukumu mahususi. Hali kadhalika, lugha ya Kiswahili na ya Kiingereza huwa na uamilifu tofauti hivi kwamba lugha ya Kiswahili huitawala lugha ya Kiingereza kwa kuiwekea muundo wa kimofosintaksia ambamo mofimu za Kiingereza huchopekwa.

Utangulizi

Uhamishaji msimbo umeshughulikiwa kwa mapana (Kachru, 1983; Myers-Scotton, 1993 na Muyskern, 1995). Kachru (1983:193) anafasili uhamishaji msimbo kama uwezo wa kuhamisha matumizi ya lugha kutoka msimbo A hadi msimbo B; na uchanganyaji msimbo kama uhawilishaji wa vipengele vya kiisimu kutoka msimbo mmoja hadi mwengine. Kulingana na Kachru (keshatajwa), uhamishaji msimbo unahu ubadilishanaji wa lugha katika viwango vikubwa vya kiisimu kama vishazi na sentensi huku uchanganyaji msimbo ukihusisha ubadilishanaji msimbo baina ya vipashio vidogo kama maneno na virai. Myers-Scotton (keshatajwa) na Muysken (keshatajwa) hutumia istilahi uhamishaji msimbo kama istilahi mwavuli inayojumuisha dhana zote mbili. Katika utafiti huu, istilahi uhamishaji msimbo inatumika kurejelea uchanganyaji wa elementi za kisarufi kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwenye sentensi moja.

Kimsingi, uhamishaji msimbo huchunguzwa kwa namna mbili kuu. Mkondo wa kwanza huoanisha masuala ya kijamii na uhamishaji msimbo na mkabala wa pili hulenga kuchunguza miundo ya kisarufi ya uhamishaji msimbo. Mkondo wa kijamii hutalii sababu na majukumu ya kubadilisha msimbo na mkondo wa kisarufi huazimia kueleza sifa za kimofolojia na kisintaksia zinazodhihirika wakati maumbo ya mifumo miwili tofauti yanapokutana kwenye sentensi moja. Utafiti huu unaegemea mkondo huu wa pili wa kisarufi kwa sababu kazi hii inalenga kuchambua mofosintaksia ya sentensi za Kiswahili-Kingereza hususani kuainisha mofimu katika sentensi husika.

Mofimu zimekuwa zikiainishwa katika makundi mawili makuu. Kwa mujibu wa Lieber (2009:34), kuna mofimu huru na mofimu fungo. Mofimu huru ni zile mofimu ambazo zinaweza kujisimamia kama neno na kujitosheleza kimaana. Mofimu fungo nazo ni zile mofimu ambazo haziwezi kujitosheleza kimaana bila kuambatanishwa na mofimu nyingine. Utafiti huu unaangalia uainishaji wa mofimu kwa namna nyingine tofauti kuegemea modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi (KLM) ya Myers-Scotton (keshatajwa) na modeli ya M-4 ya Myers-Scotton & Jake (keshatajwa). Waasisi hawa wanaainisha mofimu kutegemea hasa jukumu la mofimu husika. Kwanza, yapo makundi mawili makuu ya mofimu. Kuna mofimu za kidhana na mofimu za kimfumo. Mofimu hizi za kimfumo huainishwa tena katika makundi matatu zaidi: mofimu mfumo za mapema, mofimu mfumo za kidaraja, na mofimu mfumo za nje. Maelezo zaidi kuhusu aina hizi za mofimu yanatolewa katika sehemu ya msingi wa kinadharia.

Data ya utafiti huu ilikusanya kutoka mazungumzo ya kawaida ya vipindi viwili vilivyokuwa vikipeperushwa katika runinga ya NTV ya Kenya. Vipindi hivi ni *The Wicked Edition* na *The Real Househelps of Kawangware*. Kipindi cha *The Wicked Edition* kilipeperushwa kila siku ya Ijumaa kuanzia saa moja na nusu usiku hadi saa mbili usiku na kile cha *The Real Househelps of Kawangware* kikipeperushwa kila siku ya Jumatano kuanzia saa moja na nusu usiku hadi saa mbili usiku kila wiki. Kipindi cha *The Wicked Edition* huchukua mtindo wa mahojiano ambapo mwendesha kipindi hulenga kuibua ucheshi kwa namna anavyowahoji wageni wake. Kipindi cha *The Real Househelps of Kawangware* nacho ni mchezo wa kuigiza unaoangalia maisha ya wafanyikazi wa nyumbani, waajiri pamoja na marafiki zao.

Vipindi hivi vilichaguliwa kupitia mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi kwa sababu wale wanaohusika kwenye vipindi hivi aghalabu hutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa pamoja katika mazungumzo yao. Mazungumzo ya vipindi vitano kwa kila kipindi yalirikodiwa kisha sentensi zote zilizokuwa na mofimu za Kiswahili na Kiingereza zikanakiliwa katika karatasi. Jumla ya sentensi mia moja zilichanganuliwa. Mofimu zote kutoka lugha ya Kiingereza ziliandikwa kwa herufi ya mlazo huku zile za Kiswahili zikiandikwa kwa herufi ya kawaida. Vilevile, maumbo yote yaliyokusudiwa kuangaliwa zaidi katika maelezo, yaliandikwa kwa herufi za italic.

Utumikizaji wa modeli za KLM na M-4

Watafiti mbalimbali wamejaribu kutumikiza modeli za Kiunzi cha Lugha Msingi na M-4 kuelezea miundo mbalimbali ya kisarufi ya uhamishaji msimbo. Baadhi ya watafiti hawa wameonesha kwamba kwa kiwango kikubwa, kanuni zinazopendekezwa na modeli hizi zinaweza kutumika kuelezea data ya uhamishaji msimbo wa lugha zilizochunguzwa. Hata hivyo, watafiti wengine wamebainisha aina za miungano ya mofimu ambayo modeli hizi imeshindwa kueleza kikamilifu kama inavyojadiliwa hapa chini.

McLain-Jespersen (2014) anatumikiza Modeli ya Lugha Msingi na ile ya M-4 kuchanganua uhamishaji msimbo unaohusu Kiarabu cha Kialgeria na Kifaransa. McLain-Jespersen (keshatajwa) alichunguza ruwaza za kumuundo katika nyimbo za msanii wa nyimbo za kufoka – Lofti Double Kanon. Anabaini kwamba uhamishaji msimbo unaodhihirika kwenye nyimbo hizo unaoana na kanuni za modeli ya Lugha Msingi na ile ya M-4 kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, anatambua mifanyiko mitatu katika data yake ambayo inashindwa kuelezewa na modeli hizi kwa maana inakiuka kanuni zake. Mifanyiko hii ni pamoja na: kuwapo kwa vibainishi viwili kutoka lugha za Kiarabu cha Kialgeria na Kifaransa vikitangulia nomino ya Kifaransa. Pili, kihuishi cha Kifaransa, *jamais* (asilani) kinapohamishwa katika Kiarabu cha Kialgeria kinavuruga kanuni za mpangilio wa maneno wa Kiarabu cha Kialgeria kwa maana kihuishi hiki hakiambatani na kiambishi cha ukushaji kwa mujibu wa sarufi ya Kiarabu cha Kialgeria. Tatu, baadhi ya vitenzi vya Kifaransa vilipohamishwa katika Kiarabu cha Kialgeria,

mizizi ya vitenzi hivi iliweza kuchukua mofimu za irabu ambazo hazipatikani katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarabu cha Kialgeria na hivyo basi kuzua maneno yenyе muundo tata.

Ingawa McLain-Jespersen (keshatajwa) anatumikiza modeli za Myers-Scotton & Jake (keshatajwa), utafiti wake unatofautiana na huu wetu. Kwanza, huku utafiti wetu ukiazimia kuainisha mofimu za sentensi zinazotokana na uhamishaji msimbo wa Kiswahili na Kiingereza, McLain-Jespersen (keshatajwa) anachunguza miundo ya kiisimu ya uhamishaji msimbo wa Kiarabu cha Kialgeria na Kifaransa. Pili, data ya uchunguzi wa McLain-Jespersen (keshatajwa) inatokana na nyimbo za kufoka za msanii mmoja huku data ya utafiti huu wa sasa ikiwa ni semi zinazotokana na mazungumzo halisi kutoka katika vipindi vya runinga. Fauka ya hayo, kwa kuwa ametumia modeli hizi za kisarufi kuchunguza uhamishaji msimbo unaohusu Kiarabu-Kifaransa, basi kuna haja ya kutumia modeli hizo katika uhamishaji wa Kiswahili-Kiingereza kutathmini kufaa ama kutofaa kwake.

Maoni kama haya ya McLain-Jespersen (keshatajwa) yanashikiliwa na Nchare (2010) anapochunguza ruwaza ya mofimu za vitenzi vilivyoambishwa na pia vitenzi ambavyo havikuambishwa kutoka lugha chopekwa ambazo zilikuwa Kifaransa na Kiingereza. Nchare (keshatajwa) anachunguza uhamishaji msimbo katika lugha za Kikameruni, Kifaransa na Kiingereza. Anatumia istilahi *Camfranglais* kurejelea uhamishaji msimbo huo. Kulingana na mtafiti huyu, vitenzi vyote vilivyoambishwa vilichukua mofimu za kimfumo kulingana na kanuni zinazopendekezwa na modeli ya 4-M lakini vitenzi ambavyo havikuambishwa havikuweza kutolewa maelezo na modeli hiyo. Utafiti wa Nchare (keshatajwa) umeufaa utafiti huu kwa maana unalenga kubaini namna mofimu za lugha ya Kiswahili na Kiingereza zinavyoungana kujenga sentensi ya uhamisho msimbo. Hata hivyo, kuna tofauti kati ya utafiti wa Nchare (keshatajwa) na huu kwa maana kazi hii inalenga kuchunguza aina za mofimu zinazojenga sentensi ya Kiswahili-Kiingereza huku Nchare (keshatajwa) akitafiti uhamishaji msimbo unaotokana na mseto wa lugha za Kikameruni, Kifaransa na Kiingereza. Kuna haja ya kuchunguza mofimu katika sentensi ya Kiswahili-Kiingereza kubaini ikiwa zina sifa na dhima kama zile za uhamishaji msimbo unaohusu lugha nyingine tofauti.

Mwandije (2004) ametumikiza modeli ya Myers-Scotton (keshatajwa) ya Kiunzi cha Lugha Msingi kuchunguza data ya Kiswahili-Kiingereza kwa minajili ya kutathmini ufaafu wa modeli husika. Hii ndiyo kazi tuliyokumbana nayo ikijaribu kuchunguza data ya uhamishaji msimbo wa Kiswahili-Kiingereza kwa mkabala wa kisarufi. Matokeo ya uchunguzi wa Mwandije (keshatajwa) yalidhihirisha kwamba kwa kiasi fulani kanuni zinazopendekezwa na modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi zinaweza kutumika kutambua Kiswahili kama lugha msingi na Kiingereza kama lugha chopekwa. Hata hivyo, katika miktadha mingine, kanuni hizi zilifeli kuchambua data hii kikamilifu. Kazi ya mtafiti huyu ilitumia modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi pekee, modeli ambayo kwa sasa imepanuliwa kwa kuongezewa kanuni zaidi chini ya modeli ya M-4 ili kushughulikia uhamishaji msimbo kwa kina. Utafiti wetu unatofautiana na ule wa Mwandije (keshatajwa) kwani unalenga kuainisha mofimu za sentensi ya Kiswahili-Kiingereza kwa kutumikiza modeli mpya ya M-4. Tunatarajia kwamba, modeli hizi mbili zitawenza kuutatua ukungu aliokumbana nao mtafiti huyu. Chanzo cha ukungu huu hasa kilitokana na utumikizwaji wa kigezo cha *frikwensi* kutambua lugha msingi na vilevile, utata uliohusiana na ubainishaji wa zile mofimu za kimfumo.

Modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi

Modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi ya Myers-Scotton (keshatajwa) huchunguza miundo ya sarufi ya uhamishaji msimbo kwa kumulika majukumu yanayotekelvezwa na aina tofauti tofauti za mofimu katika sentensi. Dai kuu la modeli hii ni kwamba lugha mbili zinapotumika katika sentensi moja haziwi na jukumu wala hadhi sawa. Mojawapo ya lugha huitawala ile nyingine. Hali kadhalika, mojawapo ya lugha husika ndiyo huwa chanzo cha aina fulani za mofimu. Lugha inayotawala nyingine huitwa lugha msingi, na lugha inayotawaliwa huitwa lugha chopekwa. Lugha msingi huiwekea lugha chopekwa msingi ama kiunzi dhahania cha kimfosintaksia ambamo mofimu kutoka lugha chopekwa huingizwa. Mfano unaofuata, ambao umetoka katika data yetu, unaonesha namna lugha msingi inavyoivekea lugha chopekwa muundo wa kimfosintaksia.

1. Wewe unadhani hawa mapoliticians wanadeserve kura zetu?

Unapotazama sentensi ya (1) unaweza kuona kwamba elementi za Kiingereza *politicians* na *deserve* zinaingizwa katika mfumo ambao tayari umeshawekwa na lugha ya Kiswahili. Sentensi nzima inazingatia mpangilio wa maneno wa lugha ya Kiswahili wa Kiima+Kitenzi+yambwa. Nomino *politicians* inachopekwa katika nafasi ya nomino ya Kiswahili, “wanasiasa” baada ya kuambishwa kiambishi *ma-* cha wingi. Nomino, *mapoliticians* imo katika nafasi ya kiima cha sentensi kuu, na *wanadeserve* inaingia katika nafasi ya kiarifu. Ni dhahiri kwamba, elementi za lugha ya Kiingereza sharti ‘zitii’ kanuni za mfumo wa Kiswahili ili ‘zikubaliwe’ kwenye muundo wa sentensi husika. Kwa mfano, ingawa mofimu ya wingi huashiriwa na kiambishi –s katika Kiingereza kama ilivyo katika nomino *politicians*, bado nomino hiyo inalazimika kuchukua mofimu *ma-* ya wingi katika Kiswahili.

Modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi inatofautisha aina kuu mbili za mofimu: mofimu za kidhana na mofimu za kimfumo. Mofimu za kidhana ni zile mofimu ambazo hubeba maana ya kisemantiki. Hizi ndizo mofimu ambazo mzungumzaji huwazia kwanza anaponua kuwasilisha ujumbe wake. Mofimu hizi ni pamoja na nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, na baadhi ya vihusishi. Kwa upande mwingine, mofimu za kimfumo hazibebi maana ya kisemantiki. Jukumu la mofimu hizi ni kuonesha mahusiano ya kisarufi baina ya mofimu za kidhana. Hii ina maana kwamba, mofimu za kimfumo hutumika kudumisha muundo wa sentensi husika. Tazama sentensi ifuatayo kutoka katika data yetu:

2. Mkishaiba hamkuwa *mnafeel guilty*?

Sentensi ya (2) hapo juu ina maneno manne. Kuna vitenzi vitatu (Mkishaiba, hamkuwa, *mnafeel*) na kivumishi kimoja (*guilty*). Vipashio hivyo vinne ni mofimu za kidhana. Hata hivyo, kuna aina nyingine za mofimu ambazo ndizo zinazotekeleza majukumu ya kisarufi yakiwa ni pamoja na kuashiria habari za idadi, njeo, ukashaji na upatanisho wa kisarufi. Mofimu hizi ni pamoja na ***m* na *na*** katika kitenzi *m-na-feel* na ***ha*** na ***m*** katika kitenzi *hamkuwa*. Hizi ndizo mofimu za kimfumo. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (keshatajwa), mofimu za kimfumo huchaguliwa baada ya zile za kidhana kwisha kuwaziwa na kuteuliwa.

Ubainishaji wa lugha msingi

Modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi inapendekeza kanuni mbili ambazo zinaweza kutumika kutambua lugha msingi katika sentensi iliyohamishiwa misimbo. Kwanza, kuna kanuni ya mpangilio wa mofimu na pili ni kanuni ya mofimu za kimfumo. Kanuni ya mpangilio wa mofimu hudai kwamba vipashio kutoka katika lugha msingi na lugha chopekwa hutii mpangilio wa kisarufi wa lugha msingi. Hii ina maana kwamba ili tuweze kutambua lugha msingi, tunapaswa kwanza kuubainisha mpangilio wa maneno wa sentensi husika, kisha tutalii tabia za elementi kutoka lugha zote. Katika muktadha huu, iwapo vipashio vya Kiswahili vinafuata mpangilio wa maneno wa Kiingereza, basi Kiingereza ndiyo lugha msingi. Ikiwa elementi za Kiingereza zinazingatia mpangilio wa maneno ya lugha ya Kiswahili, basi Kiswahili ndiyo itakuwa lugha msingi. Tazama sentensi mbili zifuatazo ambazo zimetoka kwenye data yetu:

3. Mtu m-*dark* kama wewe hufai kuringa.
4. Hapa kwenu kuki-*rob*-iwa mtu wa kwanza kuwa *suspect* ni *soldier*.

Katika sentensi ya (3), kivumishi *dark* cha lugha ya Kiingereza kinafuata mpangilio wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Katika Kiswahilli, vivumishi hutanguliwa na nomino lakini katika Kiingereza ni vivumishi vinavyotangulia nomino. Aidha, katika sentensi ya (4), kitenzi *rob* kinapachikwa katika nafasi ya kitenzi cha Kiswahili. Kitenzi hiki ambacho kiasili ni mzizi wa kitenzi, kinalazimika kuchukua viambishi vya kisarufi vya Kiswahili ili kudumisha muundo na mpangilio wa viambishi katika kitenzi cha Kiswahili. Hali kadhalika, vibainishi *the* na *a* ambavyo aghalabu huandamana na nomino katika Kiingereza vinadondoshwa vinapochopewa katika muundo wa sentensi ya Kiswahili kama inavyodhihirishwa na nomino *suspect* na *soldier*. Ingekuwa sentensi ya Kiingereza, tungetaraji kuwa na virai nomino *the suspect* na *a soldier*. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba sentensi (3) na (4) zinathibitisha kwamba Kiswahili ni lugha msingi na Kiingereza ni lugha chopekwa.

Kanuni ya pili ya kutambua lugha msingi kati ya Kiswahili na Kiingereza ni kanuni ya mofimu za kimfumo. Kanuni hii hudai kwamba mofimu zote za kimfumo ambazo zina mahusiano ya kisarufi lazima zitoke katika lugha msingi (Myers-Scotton, keshatajwa). Mofimu hizi za kimfumo aghalabu hutumika kuonesha taarifa za nafsi, ukanushaji, njeo, hali, kauli,

upatanisho wa kisarufi mionganini mwa nyingine. Kwa mfano, katika sentensi ya (5) hapa chini, mofimu *tu-* na *-li-* kwenye neno *tulihijack* ni mfano wa mofimu za kimfumo ambazo zinaweza tu kutoka katika lugha ya Kiswahili. Tazama mfano ufuatao kama unavyodhihirika kutoka kipindi cha *The Wicked Edition*.

5. *Tulihijack* gari ya hii Nation ya kubeba magazeti

Ni muhali kwa mofimu ya kimfumo ya Kiingereza *-ed* ya kuashiria wakati uliopita kuingizwa katika muundo wa kitenzi cha Kiswahili. Katika muktadha wa sentensi ya (5) hapo juu, wakati uliopita wa kitenzi *hijack* ni *hijacked*. Hata hivyo, kitenzi hiki *hijacked* hakiwezi kuchukua mofimu *tu-* ya nafasi ya Kiswahili kuunda kitenzi **tuhijacked*. Sababu kuu ya kutowezekana huku ni kwamba *-ed* na *tu-* ni mofimu za kimfumo ambazo sharti zitoke kwa lugha msingi ambayo ni Kiswahili.

Modeli ya M-4

Katika mwaka wa 2000, Myers-Scotton & Jake (keshatajwa) waliipanua modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi wakaibuni modeli ya M-4. Modeli ya 4-M ina maana ya “mofimu nne” kutokana na sifa yake ya kuainisha mofimu katika makundi manne. Kama tulivyokwisha kueleza chini ya modeli ya Kiunzi cha Lugha Msingi, kuna mofimu za kidhana na mofimu za kimfumo. Modeli ya 4-M huziainisha zaidi mofimu hizi za kimfumo katika makundi matatu. Makundi haya ni pamoja na: mofimu mfumo za mapema, mofimu mfumo za kidaraja, na mofimu mfumo za nje. Uainishaji wa mofimu hizi hutegemea vigezo viwili. Kwanza, ni jukumu linalotekelawa na mofimu husika na pili, ni wakati wa kuichagua mofimu husika katika mchakato wa kuzalisha lugha. Sehemu inayofuata inazamia kwa kina uainishaji huu kwa kujikita katika sentensi zilizochambuliwa kutoka katika data yetu.

Mofimu za kidhana

Tumedokeza hapo juu kwamba mofimu za kidhana ni zile mofimu ambazo hubeba maana au wazo ambalo mzungumzaji analenga kuliwasilisha. Ni mofimu ambazo humwezesha mzungumzaji kuwasilisha ujumbe wake. Mifano mikuu ya mofimu hizi ni nomino na vitenzi.

Kutokana na umuhimu huu wa kuwasilisha wazo, mofimu za kidhana ndizo hufikiriwa na kuchaguliwa zikiwa za kwanza katika mchakato wa kuzalisha lugha (Myers-Scotton & Jake, keshatajwa). Kwa mujibu wa wataalamu hawa, mofimu za kidhana zinaweza kuchangiwa na lugha msingi ama lugha chopekwa. Tazama mfano unaofuata:

6. Jamaa alikuwa na *case ya rape* lakini si ye ye ali-*rape*

Katika sentensi ya (6), nomino *case* na kitensi *rape* ni mofimu za kidhana zinazochangiwa na lugha ya Kiingereza. Vivyo hivyo, kitensi *kuwa* na *si* ni mofimu za kidhana zinazotoka katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa mofimu za kidhana huweza kuchangiwa na mojawapo ya lugha husika, uteuzi wa mofimu (gani) itakayoteuliwa na mzungumzaji hutegemea masuala ya kijamii na ya kiisimu nafsi.

Mofimu mfumo za mapema

Mofimu mfumo za mapema ni mofimu ambazo huandamanishwa na mofimu za kidhana wakati wa mawasiliano. Ni mofimu ambazo hazibebi maana ya kileksia. Zinapotumika pamoja na mofimu za kidhana, zinakuwa na jukumu la kuongezea mofimu husika taarifa mahususi, mathalani, taarifa za idadi, ukamilifu na uwazi. Kwa kuwa mofimu hizi hubeba habari muhimu, huchaguliwa pamoja na mofimu za kidhana. Zinaitwa mofimu za mapema kwa maana huchaguliwa mapema ikilinganishwa na mofimu nytingine za kimfumo katika mchakato wa uzalishaji lugha. Lugha za Kiswahili na Kiingereza zimesheheni aina hizi za mofimu. Kwa mfano, katika Kiswahili kuna mofimu za ngeli kama vile *wa-* katika neno *wa-tu*, *vi-* katika neno *vi-tanda* na kadhalika. Katika lugha ya Kiingereza kuna vibainishi *a/the*, na mofimu *-s* ya wingi mionganoni mwa nytingine. Tazama mfano ufuatao unaotoka katika kipindi cha *The Real Househelps of Kawangware*:

7. Wewe uko *busy* hapa unashikana na *ma-housemaid*

Katika sentensi ya (7) hapo juu, nomino *housemaid* ni mofimu ya kidhana. Kiambishi awali *ma-* nacho ni mofimu mfumo ya mapema kwa maana inaongezea mofimu ya kidhana *housemaid*, habari za wingi. Wakati wa mawasiliano, mofimu hii *ma* huchaguliwa pamoja na mofimu *housemaid*. Kama zilivyo mofimu za kidhana, mofimu mfumo za mapema zinaweza

kuchangiwa na mojawapo ya lugha zinazohusika katika uhamishaji msimbo. Tazama sentensi ifuatayo kutoka katika *The Wicked Edition*:

8. Sisi ma-*hustler-s* tunateseka.

Katika sentensi ya (8), *ma-* na *-s* katika mofimu ya kidhana *hustler* ni mofimu mfumo za mapema. Mofimu *ma-* inachangiwa na lugha msingi, huku *-s* ikichangiwa na lugha chopekwa. Mofimu zote zinawasilisha taarifa ile ile moja ya wingi ingawa *ma-* ya Kiswahili inatumika kuashiria ngeli ya nomino husika. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (2002:92), ni mofimu mfumo za mapema tu za lugha tofauti zinazoweza kutumika kwa pamoja katika sentensi moja.

Mofimu mfumo za baadaye

Mofimu mfumo za baadaye hujulikana kama mofimu za baadaye kwa maana husubiri hadi pale ambapo mofimu za kidhana na mofimu mfumo za mapema zimeshachaguliwa ama kuwekwa tayari kwenye leksikoni ya akilini tayari kuanza kutamkwa. Jukumu la mofimu za baadaye ni kuunga pamoja vipashio vikubwa kama virai na vishazi. Uundaji huu wa vipashio hivi vikubwa hutekelezwa kwa njia mbili tofauti. Njia ya kwanza ni kuunganisha vipashio vilivyo ndani ya kirai ama kishazi kimoja na njia ya pili ni kudhihirisha uhusiano wa kisarufi baina ya vipashio mbalimbali vilivyo nje ya kirai ama kishazi kimoja. Njia hizi mbili za uungaji vipashio vikubwa unatupatia aina mbili za mofimu mfumo za baadaye, yaani mofimu za kidaraja na mofimu nje kwa kifupi.

Mofimu mfumo za kidaraja za baadaye

Mofimu hizi huitwa mofimu za kidaraja kwa maana hutumika kuunganisha vipashio viwili. Vipashio vinavyounganishwa vinaweza kuwa ndani ya kishazi kimoja au kuwa vishazi viwili. Mara nyingi vipashio vinavyounganishwa ndani ya kishazi huwa ni virai. Myers-Scotton & Jake (2016) wanadai kuwa ingawa mofimu hizi huweza kudokeza maana ya kisemantiki, kimsingi hazina maana ya kisemantiki zikiwa pekee. Mofimu za kidaraja hutumika hasa kuonesha muundo wa kingazi wa vipashio vinavyoungwa pamoja. Mfano wa mofimu za kidaraja ni mofimu *-a* unganifu ya Kiswahili ama *of* ya Kiingereza. Tazama mifano ifuatayo:

9. Hii *story* ya *sister* yako inaniudhi, vile ananicontrol inanibore. (Kutoka *The Real Househelps of Kawangware*)
10. Anakushika roho hivi ukitense, anajua kwamba uko na kitu marufuku (Kutoka *The Wicked Edition*)

Katika mfano wa (9), umbo *ya* ni mofimu ya kidaraja. Mofimu hii inaunganisha virai nomino viwili: “*story*” na “*sister*” ndani ya kishazi kimoja. Virai hivi viwili vinatumika kuunda kirai changamano, “*story ya sister*”. Umbo *y-a* pia ni mofimu changamano kwa maana mofimu – *a* unganifu imeambishwa umbo *y-* la ngeli ya 9. Mofimu –*a* unganifu katika sentensi ya (9) inatumika kuonesha uhusiano wa kingazi uliopo kati ya nomino *story* na *sister*. Umbo *y-* nalo si mofimu ya kidaraja bali ni mofimu mfumo ya nje kama inavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata . Katika mfano wa (9) hapo juu, kipashio *kwamba* ni mofimu *ya kidaraja* inayotumika kuunganisha vishazi viwili, yaani “Anakushika roho hivi ukitense anajua” na “uko na kitu marufuku.”

Mofimu mfumo za nje


Mofimu hizi huunganisha vipashio kwa kuonesha mahusiano ya kisarufi baina ya elementi zinazounda sentensi. Mofimu hizi huitwa mofimu za nje kwa maana hutokea nje ya viambajengo vinavyoathiri ama kuamua maumbo yake. Mfano wa mofimu hizi ni pamoja na viambishi vinavyoonesha upatanisho wa kisarufi baina ya kiima na kiarifu ama kati ya kitenzi na yambwa. Tazama mfano wa (11).

11. Kula si haki yako, lazima *uifightie*

Katika mfano wa (11), mofimu *u-* na *-i* katika kitenzi, “*u-i-fight-i-e*” ni mofimu mfumo nje. Umbo *u-* linarejelea msemewa, nafsi ya pili ambaye ameshatajwa ingawa hadhihiriki katika kishazi hiki. Zingatia kwamba, ingawa umbo *u-* linarejelea kiima, hivi vipashio viwili yaani kiima kilicho kapa na mofimu *u-* vimo katika viambajengo tofauti. Mrejelewa yuko katika kirai nomino na umbo *u-* liko kwenye kirai kitenzi. Vivyo hivyo, umbo awali *-i-* katika kitenzi linatumika kurejelea yambwa *haki*, elementi ambayo imo nje ya kiambajengo ilipo mofimu *-i-*. Katika sentensi ya (9), tumekwisha kudokeza kwamba *-a* unganifu ni mofimu ya kidaraja

ambayo huambishwa umbo y- la ngeli ya 9. Umbo la mofimu y- linaamuliwa na nomino *story* iliyo katika kirai nomino tofauti. Kwa hivyo, kwa kuwa mofimu y- inaonesha ukubaliano wa ngeli na vilevile inatokea nje ya kiambajengo kinachoamua umbo lake, basi –y ni mofimu mfumo ya nje.

Mchoro: Aina nne za mofimu



Hitimisho

Kazi hii imejikita katika kuainisha mofimu zinazounda sentensi ya Kiswahili-Kiingereza kwa kuongozwa na modeli za kisarufi za Kiunzi cha Luga Msingi na M-4 za Myers-Scotton (keshatajwa) na Myers-Scotton & Jake (keshatajwa) mtawalia. Imedhihirika kwamba, mofimu kwenye sentensi ya Kiswahili-Kiingereza zinaweza kuainishwa katika matapo manne. Kuna mofimu za kidhana, mofimu mfumo za mapema, mofimu za kidaraja, na mofimu za nje. Tumeona kwamba kila nomino ina jukumu lake na huchaguliwa wakati tofauti tofauti. Mofimu zilizo na jukumu la kisemantiki huchaguliwa kwanza na zile zenye majukumu ya kisarufi huchaguliwa baadaye. Mofimu za kidhana huwa na maana ya kisemantiki, mofimu mfumo za mapema huongezea mofimu za kidhana habari muhimu, na mofimu za kimfumo za baadaye hutumika kuunga vipashio vikubwa kama virai na vishazi pamoja na kuonesha uhusiano wa kisarufi baina ya elementi mbalimbali katika sentensi. Jambo jingine ambalo limewekwa wazi ni kwamba lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza huwa na hadhi tofauti. Lugha ya Kiswahili huitawala lugha ya Kiingereza kwa kuiwekeea muundo wa kimfosintaksia ambapo baadhi ya mofimu zake hususani mofimu za kidhana huchopekwa.

Marejleo

- Lieber, R. (2009). *Introducing morphology*. Cambridge University Press.
- McLain-Jespersen, S. (2014). *An application of the MLF and 4-M models to French-Arabic code switching in Algerian* (Unpublished masters thesis). Portland State University.
- Muysken, P. (1995). Code switching and grammatical theory. In L. Milroy & P. Muysken (Eds.), *One speaker two languages: Cross-disciplinary perspectives on code-switching*. Cambridge University Press. 177-198
- Mwandije, W. (2004). *The Matrix Language Frame Model of code-switching as applied to Kiswahili- English code-switching in Kenya*. (Unpublished masters dissertation). University of Nairobi, Kenya.
- Myers-Scotton, C. (1993). *Duelling languages: Grammatical structure in code-switching*. Oxford University Press.
- Myers-Scotton, C. (2002) *Contact linguistics: Bilingual encounters and grammatical outcomes*. Oxford University Press.
- Myers-Scotton, C., & Jake, J. (2000). Testing a model of morpheme classification with language contact. *International Journal of Bilingualism*, 4 (1), 1-8.
<https://doi.org/10.1177/13670069000040010101>
- Myers-Scotton, C., & Jake, J. (2016). Revisiting the 4-M model: Code-switching and morpheme election at the Abstract Level. *International Journal of Bilingualism*, 21, 340–366.
<https://doi.org/10.1177/1367006915626588>
- Nchare, A. L. (2010). *The morphosyntax of Camfranglais and the 4-M model* (Masters thesis). New York University, Department of Linguistics.